MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA

# Mfuko wa ELIMU

OKTOBA - DESEMBA, 2023

Toleo la **KWANZA**

# DKT. KIPESHA ABAINISHA FAIDA ZA KUCHANGIA MFUKO WA ELIMU WA TAIFA





- WANAFUNZI WAHIMIZWA KUPENDA MASOMO YA SAYANSI
- FANYENI KAZI KWA KUJITUMA.

*Changia Mfuko wa Elimu;*
*Boresha Miundombinu ya Elimu*

officialteatz


# KUHUSU TEA

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)** ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.

## Mfuko wa Elimu

Mfuko wa Elimu unapokea rasilimali zote ambazo hukusanywa na kuratibiwa na Mamlaka ya Elimu Tazania (TEA) kwa lengo la kufadhili miradi ya elimu nchini kutoka vyanzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. TEA imepewa jukumu la kuhamasisha rasilimali kutoka kwa wadau mbalimbali nchini na nchi za nje kwa lengo la kusaidia juhudi za Serikali kuinua ubora, na kuongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa.



## Dira

Kuwa Mfuko wa Elimu bora wenye hadhi ya kimataifa unaotatua changamoto za elimu nchini, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika kuchangia maendeleo endelevu nchini.

## Dhamira

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi katika kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu bora na ujuzi kwa usawa.

## YALIYOMO


Kuhusu TEA................................................ i

Salaam za Mkurugenzi Mkuu ........................1

1. Dkt. Kipesha Abainisha Faida za Kuchangia Mfuko wa Elimu wa Taifa...........2

2. Prof. Nombo Akutana na Wanufaika wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) ...........3

3. Fanyeni Kazi Kwa Kujituma - Dkt. Kipesha. ....4

4. Camara Education Tanzania yatoa Kompyuta zenye Thamani ya Sh. Milioni 37 Kupitia TEA...............................5

5. Wanafunzi Wahimizwa Kupenda Masomo ya Sayansi .........................................6

6. TEA Yashiriki Maadhimisho ya Miaka 50 ya NECTA .............................................7

7. TEA, Nissan Tanzania Wakabidhi Jozi 200 za Viatu kwa Wanafunzi 200 Kutoka Familia Duni Bagamoyo ...........................8

8. Watumishi wa TEA Wawashika Mkono Watoto Yatima.......................................9

10. TEA Yatembelea Eneo Lililoathirika kwa Mafuriko - Hanang ................................9



### Timu ya Uhariri:

**Mwenyekiti:** Masozi Nyirenda

**Mhariri:** Bestina Magutu

**Wachangiaji:** - Hamza Hassan
- Eliafile Solla
- Joyce Minja



*Anuani:*

**Mamlaka ya Elmu Tanzania(TEA)**

S. L.P 2516, Dodoma- Tanzania

Barua pepe: info@tea.or.tz,

Tovuti www.tea.or.tz,

Instagram: Officialteatz,


## *Salaam za Mkurugenzi Mkuu*



Nafurahi kuwakaribisha katika chapisho la kwanza la Jarida la Mfuko wa Elimu.

Jarida hili litachapishwa katika kila robo ya mwaka likionyesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) yenye jukumu la kisheria la kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu.

Mfuko huu una wajibu wa kisheria wa kukusanya raslimali kwa ajili ya kuongeza nguvu za Serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa

Nichukue fursa hii kuwashukuru wadau wote wanaochangia maendeleo ya sekta ya Elimu nchini. Kupitia michango hii tunasaidia uboreshaji wa sekta ya elimu ambayo ni chachu ya maendeleo ya nchi. TEA kama mratibu wa Mfuko wa Elimu wa Taifa inatambua michango hiyo na kuitahamini.

TEA inawakaribisha wadau wote wa elimu kutoa michango hiyo kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa. Kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa mchangiaji anaiwezesha Serikali kuratibu na kuwa na takwimu sahihi ya wachangiaji wa sekta ya elimu nchini.

Aidha, mchangiaji kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa anatambuliwa rasmi na kuingizwa kwenye rejesta ya Kudumu ya wachangiaji wa Mfuko ya Elimu sanjali na kupewa Hati ya Utambuzi wa Uchangiaji wa Elimu inayofahamika kama Certificate of Education Appreciation (CEA).

Mchangiaji anaweza kutumia cheti hicho kuomba nafuu ya kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa Kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 marejeo ya mwaka 2019.

Mamlaka inawahikikishia wachangiaji wa Mfuko wa Elimu kuwa miradi wanayofadhili kupitia Mfuko inaendeshwa kwa ufanisi na weledi.

**Dkt. Erasmus Kipesha**

*Mkurugenzi Mkuu - TEA.*

# DKT. KIPESHA ABAINISHA FAIDA ZA KUCHANGIA MFUKO WA ELIMU WA TAIFA



*Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha akizungumza na Wajumbe wa Jukwaa la Wahariri kuhusu utekelezaji na mafanikio ya TEA.*

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Dkt. Erasmus Kipesha ametaja faida za mchangiaji wa maendeleo ya elimu kupitia Mfuko wa Elimu kuwa ni pamoja na kupata Hati ya Utambuzi wa Uchangiaji wa Elimu (Certificate of Educational Appreciation) kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001.

Akizungumza na wajumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) kwa lengo la kuelezea utekelezaji wa majukumu na mipango ya TEA katika kutoa huduma kwa umma kupitia ufadhili wa miundombinu ya elimu, ametaja faida nyingine ni mchangiaji anaweza kutumia Hati ya Utambuzi wa Uchangiaji wa Elimu kuomba nafuu ya kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa Kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 marejeo ya mwaka 2019

Aidha mchangiaji wa Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamwa na TEA atatangazwa na kutambuliwa kitaifa, ambapo mchangiaji huandikwa katika rejesta ya kudumu ya wachangiaji wa elimu.

Mkutano huo ulioratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina na kufanyika tarehe 20 Novemba 2023, katika ukumbi wa mikutano wa NSSF Mavuno House Ilala Dar es Salaam, ni sehemu ya jitihada za Serikali kuelezea huduma inazozitoa kwa wananchi kupitia taasisi zake.

Mkurugenzi Mkuu wa TEA alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023 jumla ya michango na ufadhili wa Sh.1.4 imekusanywa kutoka kwa wadau mbali mbali ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Taasisi ya Asilia Giving inayojihusisha na shuguli za utalii Jijini Arusha pamoja na Taasisi ya Flaviana Matata.

Aidha katika mkutano huo wahariri wameelezwa kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Mamlaka ya Elimu Tanzania imepanga kufadhili jumla ya miradi 82 ya kuboresha miundombinu ya elimu katika shule za Msingi na Sekondari kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini. Miradi hii itakapokamilika itanufaisha wanafunzi 39,484 na walimu 169 katika shule za msingi na sekondari nchini.

Miradi itakayofadhiliwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa 82, matundu ya vyoo 336, mabweni 10, ujenzi wa maabara 18 za masomo ya sayansi na nyumba za walimu 32.



*Mhariri wa Times FM, Tausi Mbowe akiuliza maswali katika mkutano baina ya TEA na Jukwaa la Wahariri wa vyombo vya Habari uliofanyika Jijini Dar es Salam Mhariri wa Times FM, Tausi Mbowe akiuliza maswali katika mkutano baina ya TEA na Jukwaa la Wahariri wa vyombo vya Habari uliofanyika Jijini Dar es Salam.*

# PROF. NOMBO AKUTANA NA WANUFAIKA WA MFUKO WA KUENDELEZA UJUZI (SDF)



*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo (katikati) akimsikiliza mmoja wa wanufaika wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) alipotembelea banda la TEA kwenye maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika Kibaha Mkoani Pwani.*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), Prof. Carloyne Nombo amefurahishwa na namna wanufaika wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi (SDF) yaliyokuwa yanaratibiwa na TEA walivyoweza kutumia ujuzi waliopata kuzalisha bidhaa mbali mbali kwa ajili ya kujipatia kipato.

Prof. Nombo amesema hayo wakati wa maadhimisho ya kilele cha Juma la Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika kuanzia tarehe 9 hadi 13 Oktoba 2023 Wilayani Kibaha, Mkoani Pwani, ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Prof. Adolf Mkenda Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST).

Akiwa katika banda la TEA, Prof. Nombo alikutana na baadhi ya wanufaika wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi yaliyotolewa kupitia ruzuku ya Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) uliofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Benki ya Dunia.

Prof. Nombo amesema ni jambo la kufurahisha kuwaona wanufaika wa SDF wamethubutu kufanyia kazi kile walichojifunza na kuzalisha bidhaa na kwamba ni wakati muafaka kuzitangaza bidhaa hizo ili kukuza soko. Zaidi ya Watanzania 49,000 wamenufaika na ufadhili wa mafunzo ya SDF.

*"Hizi bidhaa mnazozalisha ni nzuri na nina uhakika zina soko kubwa tuu hapa nchini, andaeni mikakati ya kuzitangaza ili ziwafikie watanzania wengi zaidi"* amesema Prof. Nombo.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), ilishiriki maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi ambao unatoa Mafunzo ya Ujuzi kwa lengo la kuwasaidia Watanzania kujihusisha kwenye shughuli za uzalishaji mali ili kujikwamua kiuchumi.

Viongozi mbalimbali walipata fursa ya kutembelea banda la TEA akiwemo Naibu Katibu Mkuu Ofisi Rais TAMISEMI anayehusika na masuala ya Elimu Bw. Charles Msonde na kujionea bidhaa zinazozalishwa na wanufaika wa Mafunzo ya SDF.



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI (Elimu) Dkt. Charles Msonde ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi ya TEA akizungumza na mmoja wa wanufaika wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) alipotembelea banda la TEA kwenye maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika Kibaha Mkoani Pwani.*

# FANYENI KAZI KWA KUJITUMA - DKT. KIPESHA.



*Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha akipokelewa na watumishi wa TEA ofisi ya Dar es Salaam mara baada ya Kuteuliwa kushika nafasi hiyo.*

Watumishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) wamekumbushwa kufanya kazi kwa bidii na kujituma ili kufikia malengo yanayotarajiwa na Serikali na umma wa watanzania kuhusu TEA.

Kauli hii ameitoa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka Dkt. Erasmus Kipesha mara baada ya kuwasili katika ofisi za TEA Jijini Dodoma na kuwa na kikao kifupi na watumishi kufuatia uteuzi wake katika nafasi hiyo uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan mnamo tarehe 23 Septemba 2023.

Akizungumza kwa niaba ya watumishi Meneja wa Huduma za Sheria wa TEA, Bi Christina Meela, amempongeza Dkt. Kipesha kwa uteuzi na kumhakikishia kuwa watumishi wako tayari kushirikiana nae ili kufanikisha majukumu ya Mamlaka lakini pia kutekeleza malengo ya Serikali.



*Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi katika ofisi za TEA -Dar es Salaam.*

# CAMARA EDUCATION TANZANIA YATOA KOMPYUTA ZENYE THAMANI YA SHILINGI MILIONI 37 KUPITIA TEA

Shirika la Camara Education Tanzania limetoa msaada wa Kompyuta 100 zenye thamani ya Sh. Milioni 37 kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaoratibiwa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ambayo ina jukumu la kisheria la kukusanya michango kwa ajili ya sekta ya elimu nchini.

Kompyuta hizo 100 zimetolewa kwa shule nne za Sekondari zilizoko kwenye Mikoa ya Tanga na Pwani ambapo kila shule imepata Kompyuta 25 kwa lengo la kuwezesha wanafunzi kupata masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi kompyuta hizo iliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Semkiwa Wilayani Korogwe Mkoani Tanga tarehe 23 Agosti 2023, aliyekua Mkuu wa Wilaya hiyo Mhe. Jokate Mwegelo aliwahimiza wanafunzi kusoma kwa bidii kutokana na kuwekewa mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia.

*"Namna pekee mnayoweza kuonyesha shukrani kwa wafadhili walioleta msaada shuleni kwenu ni kusoma kwa bidii na kuendelea kufanya vizuri katika masomo yenu".* Amesema Mwegelo.

Katika hafla hiyo, shule ya Sekondari Semkiwa ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe na Shule ya



*Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe Jokate Mwegelo (kushoto) akipokea Kompyuta kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi Masozi Nyirenda katika hafla ya kukabidhi kompyuta kwa ajili ya shule za Sekondari za Mkoa wa Tanga.*

Sekondari Kwaluguru ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni zimekabidhiwa Kompyuta 25 kila moja.

Kwa upande wa Mkoa wa Pwani wanufaika ni Shule ya Sekondari Rafsanjani Soga iliyopo katika Halmashauri ya Mji Kibaha na Shule ya Sekondari Simbani iliyopo katika Halmashauri ya Kibaha ambapo kila shule itapata Kompyuta 25.

Mwakilishi wa Camara Education Tanzania, Bi. Asia Bonanga amesema shirika la Camara Education Tanzania, linajikita katika kupeleka teknolojia ya mawasiliano mashuleni ili kusaidia jitihada za kupatikana kwa elimu bora nchini.

Ameongeza kuwa maono ya Camara Education Tanzania ni kuona hakuna mwanafunzi anayeachwa nyuma katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano - TEHAMA.

Kaimu Mkurugenzi wa Miradi na Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi kutoka TEA, Bw. Masozi Nyirenda ameshukuru Shirika la Camara Education Tanzania kwa msaada huo wa Kompyuta na kukumbusha shule zilizonufaika kuzitumia na kuzitunza vizuri ili zidumu na kunufaisha kundi kubwa la wanafunzi.

*"Kama tunavyofahamu vifaa hivi vinahitaji utunzaji maalum ikiwa ni pamoja na kuwa na vyumba vinavyofaa, hivyo shule nufaika zijiandae vyema kwa hili"* ameongeza Bw. Nyirenda.

TEA ni Taasisi ya umma inayofanya kazi chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa inafadhili ujenzi wa miundombinu ya elimu ikiwemo madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo, mabweni, mabwalo na majiko yake, maabara na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote za elimu Tanzania Bara na ngazi ya Elimu ya Juu.



*Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe Jokate Mwegelo (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uendeshaji wa Shirika la Camara Education Tanzania, Bw. Godfrey Ezekiel wakati wa hafla ya kukabidhi kompyuta kwa ajili ya shule za Sekondari za Mkoa wa Tanga.*

# WANAFUNZI WAHIMIZWA KUPENDA MASOMO YA SAYANSI

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Maulilio Kipanyula amewahimiza wanafunzi wa kitanzania kupenda masomo ya sayansi na teknolojia kutokana na mchango wake katika kuleta maendeleo ya nchi.




*Aliyekuwa Mkurugenzi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Maulilio Kipanyula (wa pili kulia mstari wa mbele) akipokea jarida la OYLA Africa kutoka kwa Mkurugenzi wa Baobab Shalom Limited Bw. Yev Semikov (wa pili kushoto).* ***Majarida hayo yanalenga kuhimiza wanafunzi kusoma masomo ya Sayansi, Teknolojia na Hisabati.***

Prof. Kipanyula amesema Sayansi na Teknolojia imeleta mapinduzi makubwa kitaifa na kimataifa na hasa katika sekta za elimu, habari, biashara na huduma mbali mbali za kijamii.

Ameongeza kuwa Serikali ya awamu ya sita imeweka kipaumbele katika sekta ya elimu ambapo imewekeza kwa kiwango kikubwa ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vya kujifunzia na kufundishia hivyo kuwahamasisha wanafunzi kujifunza kwa bidii na kuwa wabunifu.

Alikuwa akizungumza katika hafla fupi ya kugawa majarida 700 yanayofahamika kama OYLA Africa ambayo yametolewa na kampuni ya Baobab Shalom Limited ya jijini Dar es Salaam kufuatia Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) yaliyosainiwa kati ya Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bi. Bahati Geuzye na Mkurugenzi wa Kampuni ya Baobab Shalom Limited, Bw. Yev Semikov.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Baobab Shalom Limited, Bw. Semikov amesema lengo la Majarida hayo ni kuwezesha wanafunzi wanaoyatumia kuwa wabunifu na wadadisi kwa lengo la kuboresha mazingira na maisha yao kwa ujumla.

TEA imeshukuru kampuni ya Baobab Shalom Limited kwa kutoa msaada huo wa majarida kupitia Mfuko wa Elimu unaosimamiwa na TEA na kuongeza kuwa iko tayari wakati wote kushirikiana na wadau wa elimu na kuwahakikishia kuwa misaada ya elimu inayopita kwenye Mfuko wa Elimu wa Taifa inasimamiwa kikamilifu na kutumika kama ilivyokusudiwa.




*Baadhi ya wanafunzi katika picha ya pamoja na Mgeni Rasmi wakiwa wameshika magazeti ya OYLA Africa yaliyotolewa Kampuni ya Baobab Shalom Limited ya jijini Dar es Salaam.*

# TEA YASHIRIKI MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA NECTA




*Afisa Miradi kutoka TEA Bi. Mwafatma Mohamed akitoa Elimu kuhusu kazi zinazotekelezwa na TEA katika Maonesho ya miaka 50 ya Baraza la Mitihani la Tanzania Jijini Dar es Salaam.*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni miongoni mwa taasisi za umma zilizoshiriki maonyesho ya maadhimisho ya miaka 50 ya Baraza la Mitihani Nchini (NECTA) yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Novemba hadi tarehe 3 Desemba 2023.

Akizungumza na wadau wa masuala ya Elimu katika kilele cha maonyesho ya maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Baraza la Mitihani Tanzania Mkurugenzi Mkuu wa TEA Dkt. Erasmus Kipesha amesema, maendeleo ya elimu yataletwa na watanzania wenyewe kwa kuchangia rasilimali fedha ama vifaa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa .

Dkt. Kipesha alifafanua kuwa mchangiaji anaweza kuwa mtu yeyote anayetoa udhamini au ruzuku kwa wanafunzi mbali na watoto wake, familia yake au mwajiriwa wake, kwa lengo la kuwasaidia kuendelea na elimu kwenye ngazi ya sekondari au elimu ya juu ambapo udhamini huo atautoa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa.

# TEA, NISSAN TANZANIA WAKABIDHI JOZI 200 ZA VIATU KWA WANAFUNZI 200 KUTOKA FAMILIA DUNI BAGAMOYO

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na kampuni ya NISSAN Tanzania wamekabidhi jozi 200 za viatu kwa wanafunzi 200 wahitaji katika Wilaya ya Bagamoyo Mkoani Pwani.

Akizungumza Agosti 10,2023 wakati wa zoezi hilo la makabidhiano katika shule ya Msingi Mtakuja, Meneja Rasilimali Watu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bi. Alice Lukindo amesema TEA itaendelea kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuendeleza elimu kusaidia sekta ya elimu nchini.

Amesema lengo ni kuwawezesha wanafunzi kutimiza malengo yao kwenye elimu na kwamba imekuwa ikipata wafadhili mbalimbali ambao wamekuwa wakisaidia kwenye Nyanja mbalimbali za elimu.

"Msaada huu utaleta hamasa kwenye masomo yao na pia kuwaepusha na maradhi mbalimbali na tumeambiwa kwamba shule hizi zinafanya vizuri sana kitaaluma kwa hiyo tunaomba muwe makini na masomo," alisema.

Kwa upande wake Ofisa Maendeleleo ya Jamii Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, Bi. Delvin Maleko, ambaye alimuwakilisha Afisa Elimu wa Bagamoyo, amewataka wazazi na walezi kwa ujumla kuchanga kwaajili ya chakula cha watoto wao pindi wakiwa shuleni.

"Katika shule zote za Bagamoyo ni shule yenu tu ambayo watoto hawapati chakula shuleni, maji yapo limeni mboga mboga watoto wale shuleni na kwa ufaulu walionao inamaana watafanya vizuri sana kwenye mitihani ya kitaifa," alisema

Nae Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mtakuja iliyoko Kata ya Fukayosi Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, Pascal Kitando ameishukuru TEA kwa kuhakikisha wamepata msaada wa viatu kwa wanafunzi ambao wanaishi kwenye familia za hali duni.

Pamoja na hayo amewaomba wadau mbalimbali kusaidia ujenzi wa uzio ili kukwepa uvamizi wa wanyama ambao wamekuwa wakisababisha uharibifu wa mali za shule.




*Kampuni ya NISSAN TANZANIA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania wakikabidhi viatu vya shule kwa watoto wanaosoma katika mazingira magumu Wilayani Bagamoyo, Mkoani Pwani.*

# WATUMISHI WA TEA WAWASHIKA MKONO WATOTO YATIMA



*Sehemu ya mahitaji yaliyokabidhiwa kwa watoto yatima katika kitua cha CHAKUWA kilichopo Sinza, Dar es Salaam.*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imetoa msaada kwa watoto yatima katika kituo cha CHAKUWAMA kilichopo Sinza jijini Dar es Salaam katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika 19 Julai 2023.

Msaada huo ambao umejumuisha michango ya watumishi wa TEA imelenga kuonyesha upendo na uwajibikaji kwenye masuala ya kijamii.

Akipokea msaada huo mlezi wa kituo hicho Bw. Hassan Khamis ameishukuru TEA kwa kuona umuhimu wa watoto yatima na kuwapa msaada ikiwa ni pamoja na vifaa vya shule kama madaftari, kalamu na mabegi.

Amesema vifaa hivyo vya shule vimepokelewa kwa wakati muafaka wakati shule zinafunguliwa na watoto hao walikuwa na uhitaji wa vifaa hivyo vya kujifunzia. Msaada huo wenye thamani ya Shilingi 1,500,000/= pia umejumuisha vyakula, magodoro na vifaa vya usafi ili kuwasadia kutunza mazingira.

# TEA YATEMBELEA ENEO LILILOATHIRIKA KWA MAFURIKO – HANANG

Ujumbe wa Mamlaka ya Elimu (TEA) umefika eneo lililoathirika na mafuriko wilayani Hanang-Mkoani Manyara tarehe 3 Desemba 2023 kwa lengo la kuona namna itakavyoshiriki kuimarisha miundombinu ya elimu iliyoathirika na mafuriko katika eneo hilo.

Ujumbe huo uliongozwa na Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Masozi Nyirenda tarehe 14 Desemba 2023, ulikutana na kuzungumza na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kisha kutembelea shule za eneo lililokumbwa na mafuriko.



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu K. Kijaji (Kushoto) akimsikiliza Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Masozi Nyirenda (kulia) katika moja ya kambi za waathirika wa maafa ya mafuriko yaliyotokea Wilayani Hanang Mkoani Manyara Desemba 3, 2023.*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)
S.L.P. 2516, Dodoma, Tanzania.

info@tea.or.tz www.tea.or.tz officialteatz

*Changia Mfuko wa Elimu;*
*Boresha Miundombinu ya Elimu*